



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI**



**TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI**

**UCHAGUZI MDOGO WA MADIWANI KATIKA KATA  
THELATHINI NA SABA (37) ZA TANZANIA BARA**

Tume ya Taifa ya Uchaguzi imepokea taarifa ya uwepo wa nafasi wazi za udiwani kutoka kwa Waziri mwenye dhamana na Serikali za Mitaa, ambaye kwa kuzingatia kifungu cha 13(1) cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, ameitaarifu Tume uwepo wa nafasi wazi za Madiwani katika Kata thelathini na saba (37) zilizopo katika Halmashauri ishirini na saba (27) na Mikoa kumi na tatu (13) ya Tanzania Bara.

Nafasi wazi za udiwani katika Kata hizo zimetokana na sababu mbalimbali zikiwemo Vifo, Kujiuzulu na kwa baadhi ya Madiwani kufutwa uanachama wa vyama vyao vya siasa.

Baada ya kupokea taarifa hiyo na kwa kuzingatia masharti ya kifungu cha 13(3) cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa; Tume ina utaarifu Umma kuhusu kuwepo kwa Uchaguzi mdogo katika Kata hizo thelathini na saba (37).

Hivyo, Tume imepanga kuendesha Uchaguzi mdogo katika Kata hizo kwa kuzingatia Ratiba ifuatayo.

1. Fomu za Uteuzi wa Wagombea zitatolewa kati ya tarehe **15 hadi 21 Septemba, mwaka huu,**
2. Uteuzi wa Wagombea utafanyika tarehe **21 Septemba, mwaka huu,**
3. Kampeni za Uchaguzi zitafanyika kuanzia tarehe **22 Septemba hadi tarehe 12 Oktoba mwaka huu,** na

4. Siku ya Uchaguzi itakuwa ni tarehe **13 Oktoba mwaka huu.**

### KATA ZENYE UCHAGUZI

NA	MKOA	NA	HALMASHAURI	NA	KATA
1	ARUSHA	1	Halmashauri ya Wilaya ya Monduli	1	Monduli Mjini
		2	Halmashauri ya Wilaya ya Meru	2	King'ori
				3	Kikwe
				4	Majengo
		3	Halmashauri ya Wilaya ya Karatu	5	Endamaghan
				6	Qurus
		4	Halmashauri ya Wilaya ya Longido	7	Namanga
2.	DAR ES SALAAM	5	Halmashauri ya Manispaa ya Kigamboni	8	Mji Mwema
		6	Halmashauri ya Manispaa ya Ilala	9	Kiwalani
3.	GEITA	7	Halmashauri ya Mji wa Geita	10	Nyankumbu
4.	KAGERA	8	Halmashauri ya Manispaa ya Bukoba	11	Kagondo
				12	Hamugembe
5.	KIGOMA	9	Halmashauri ya Wilaya ya Kakonko	13	Rugenge
				14	Katanga
6.	KILIMANJARO	10	Halmashauri ya Wilaya ya Same	15	Vumari
		11	Halmashauri ya Manispaa ya Moshi	16	Korongoni
		12	Halmashauri ya Wilaya ya Siha	17	Ndumeti
		13	Halmashauri ya Wilaya ya Hai	18	Romu
				19	Masama Rundugai
7	LINDI	14	Halmashauri ya Wilaya ya Liwale	20	Kibutuka

NA	MKOA	NA	HALMASHAURI	NA	KATA
8	MANYARA	15	Halmashauri ya Mji wa Babati	21	Sigino
9.	MBEYA	16	Halmashauri ya Wilaya ya Busokelo	22	Kambasegela
		17	Halmashauri ya Wilaya ya Mbalali	23	Ruiwa
10.	MWANZA	18	Halmashauri ya Jiji la Mwanza	24	Mabatini
11.	NJOMBE	19	Halmashauri ya Wilaya ya Makete	25	Kigala
12.	PWANI	20	Halmashauri ya Wilaya ya Kibaha	26	Ruvu
				27	Magindu
		21	Halmashauri ya Wilaya ya Mkuranga	28	Kisiju
				29	Njianne
		22	Halmashauri ya Wilaya Mafia	30	Kilindoni
				31	Jibondo
		23	Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji	32	Ikwiriri
		24	Halmashauri ya Mji wa Kibaha	33	Mailimoja
				34	Mbwawa
		25	Halmashauri ya Wilaya ya Kibiti	35	Ruaruke
13.	RUKWA	26	Halmashauri ya Wilaya ya Kalambo	36	Nambwenkoswe
		27	Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga	37	Ikozi

Kwa taarifa hii, Tume inavialika Vyama vya Siasa, Wadau wote wa Uchaguzi na Wananchi kwa ujumla kushiriki katika Uchaguzi huo.

**Mwisho**, Tume inachukua fursa hii kuviasa Vyama vya Siasa na Wadau wote wa Uchaguzi kuzingatia matakwa ya Katiba, Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Kanuni za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa (Madiwani) za mwaka 2015, Maadili ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani ya mwaka 2015 pamoja na

maelekezo yote yaliyotolewa au yatakayotolewa na Tume wakati wote wa Uchaguzi mdogo.

Imetolewa leo tarehe 13 Septemba, 2018.

Jaji (Rufaa) Semistocles S. Kaijage

**MWENYEKITI**

**TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI**